## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS
## OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI
## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
## SHULE YA SEKONDARI DAR ES SALAAM GIRLS

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DAR ES SALAAM GIRLS MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA …………….

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………
S.L.P ............................................
....................................................

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO (V) …………….</u>**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa binti yako amechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari ya **DAR ES SALAAM GIRLS (DGSS)**. Hii ni shule ya wasichana ya bweni ambayo ipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Kata ya Kwembe, mtaa wa Njeteni. Ipo kilometa 2.4 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo (Luguruni). Shule ya Sekondari Dar es salaam Girls ina Tahasusi za **PCM**, **PCB, CBN, na CBG.**

**MAELEKEZO YA KUFIKA SHULENI.**

Kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa umma, ukitokea Mbezi, panda daladala inayoelekea Kibamba au Mloganzila, shuka kituo cha Chuo cha St.Joseph karibu na kituo cha Mafuta Kisha panda pikipiki (1,000) itakayokufikisha shuleni. Pia kwa wenye usafiri binafsi, Ukitokea Mbezi kuelekea Kibamba nenda hadi Trafic lights za kituo cha Luguruni kunja kushoto elekea upande ilipo ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, kisha fuata njia ya vumbi mpaka kwenye kibao kilichoandikwa Njeteni Street, fuata uelekeo wa Barabara hiyo, itakufikisha shuleni.

Kwa weny usafiri binafsi wanaotokea Kibaha au Kibamba, fika eneo la Traffic Lights za Luguruni hamia upande wa kulia ili uzifikie Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Ubungo. Fuata barabara ya vumbi kama unaelekea Mbezi utakutana na kibao kilichoandikwa Njeteni Street kisha fuata uelekeo wa Barabara hiyo itakufikisha shuleni. Kwa wanaopanda usafiri wa Umma kutokea Kibaha, shuka kituo cha St.Joseph (Chuo) vuka barabara upande wa kituo cha mafuta (SHELL) panda pikipiki (1,000) itakufikisha shuleni. **KARIBU SANA**

Wanafunzi wanatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............ kuanzia saa tatu kamili asubuhi **(03:00)**. Masomo yataanza rasmi tarehe **.................**

**MUHIMU SANA**. Wanafunzi watakaofika siku 14 baada ya shule kufunguliwa bila sababu za msingi hawatapokelewa. Binti yako atatakiwa kukamilisha taratibu zifuatazo kabla ya kusajiliwa shuleni

## 1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

**MUHIMU SANA:** ***KWA MWANAFUNZI ASIYEKUWA NA BIMA YA AFYA NI LAZIMA AJE NA SHILINGI 50,400/= KWA AJILI YA KUWAKATIA BIMA YA AFYA. FEDHA HIZO ZIWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE NO: 0150796301000 CRDB JINA DAR ES SALAAM GIRLS SECONDARY SCHOOL.***

**Michango ya Shule**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MALIPO YA MICHANGO YA SHULE (80,000) YAFANYWE KWENYE ACCOUNT YA SHULE No 0150796301000 CRDB, JINA LA ACCOUNT NI DAR ES SALAAM GIRLS SEKONDARI. JINA LA MLIPAJI LIANDIKWE LA MWANAFUNZI, SIKU YA KURIPOTI SHULENI, MWANAFUNZI AJE NA STAKABADHI YA MALIPO YA MICHANGO YA SHULE AMBAYO IMETOLEWA NAKALA.**

a) **SARE ZA SHULE**
Sare za darasani ni kitambaa cha “LIGHT BLUE” na shati jeupe mikono mifupi. Sare za shule zinapatikana kwenye duka lililoko jirani na shuleni.

| |
|---|
| SKETI DRAFT AU CHECKS YENYE RANGI YA ZAMBARAU NA DAMU YA MZEE (MAROON) MSHONO LINDA BOX MBELE NA NYUMA, UREFU WA KUVUKA MAGOTI KWENYE KIFUNDO CHA MGUU. |
| MASHATI MAWILI (MIKONO MIFUPI) |
| SOKSI NYEUPE |
| SWETA MOJA (RANGI YA BLUU ILIYOKOLEA) |
| T-SHIRT MOJA YA KIJIVU YENYE NEMBO YA SHULE |

| | |
|---|
| T-SHIRT MOJA DARK BLUU ROUND YENYE NEMBO YA SHULE |
| JEZI MOJA YA JUU YA RANGI YA ZAMBARAU |

**N:B Wanafunzi wa Kiislam wanaruhusiwa kushona HIJABU nyeupe, sketi ndefu ya** DRAFT AU CHECKS **na nusu kanzu.**

b) **Sare ya michezo**

- Trucksuit ya kijani kibichi na jezi moja ya juu ya rangi ya zambarau
- Raba nyeupe.

c) **Sare ya Usiku**

- Trucksuit ya dark blue na T-shirt ya dark blue ya kusomea usiku.

d) **Shamba Dress**

- Gauni rangi ya "Zambarau" mshono wa solo, shingo ya duara, mikono mifupi.

e) **Viatu vya shule** ni vyeusi vya kudumbukiza vya kike vyenye uwazi juu (Juma na Roza).
Viatu vya plastic au viatu vya aina nyingine havitaruhusiwa darasani.




## MAHITAJI MENGINE:

### 2. MAHITAJI YA KITAALUMA:

i. Kitabu angalau kimoja kwa kila somo miongoni mwa masomo yaliyopo kwenye mchepuo husika.Tazama Kiambatisho D Vitabu vilivyopendekezwa.ii. Ream 02 ya karatasi (photocopy A4)

iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology
iv. Lab coat nyeupe kwa wanafunzi wot
v. Scientific calculator kwa wanafunzi wote

vi. Spring file 01
vii Stop watch kwa wanafunzi wa PCM na PCB
viii. Counter books 6 (quire 3 au 4 ).
ix. Madaftari madogo ya kurasa 200 yasiyopungua 8 kwa ajili ya mazoezi.
x. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
xi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na mahitaji mengine muhimu ya taaluma.
xii. kwa wanafunzi wa CBG waje na MAP SHEET BOOK (Kitabu cha ramani)
xiii. Mathematical set
xiv Begi la rangi nyeusi la kubebea na kutunzia madaftari darasani

### 3. MAHITAJI YA BWENI

i. Godoro futi 3 kwa 6 (Jipya)
ii. Mashuka 2 na foronya (rangi ya pink), chandarua cha rangi nyeupe cha pembe nne futi nne kwa sita (6x4) na balanket kwa wenye changamoto ya kiafya.
iii. Mto wa kulalia
iv. Tochi au taa ya kutumia mionzi ya jua.
v. Dettol ya maji

**4. MAHITAJI BINAFSI**

i. Taulo 1, jozi moja vitenge (nguo zisizotajwa haziruhusiwi).
ii. Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe na kijiko (vya mfupa) plastiki na udongo haviruhusiwi.
iii. Chupa ya maji ya kunywa

Sabuni za kuogea na kufulia za kutosha, mswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka na ya nywele na losheni isiyo na harufu kali, deodorant (pafume na spray haziruhusiwi), taulo za kike, taiti na sindiria iwe nyeupe au nyeusi, chupi zisizopungua 6.

iv. Sanduku la chuma na kufuli (Trunker).
v. Jozi moja ya kandambili (mpya) na pea moja ya viatu vya wazi (open shoes) au yeboyebo
vi. Nguo mbili za kulalia usiku (night dress aina ya pajama) za rangi ya blue.
vii. Pesa za matumizi madogo madogo zisizozidi shilingi 50,000/= (ambazo kwa usalama zitatunzwa na Matron)
viii Ndoo kubwa moja na ndogo moja zenye mifuniko kwa matumizi yake binafsi

**5. VIFAA VYA USAFI KWA MATUMIZI YA SHULE**

i. Ndoo ndogo moja yenye mfuniko.
ii. Kwanja 1 (Slasher lililonolewa)
iii. Fagio laini la ndani (Soft broom)
iv. Squeezer 1(kibandizio)
v. Mopa kubwa na ndoo yake
vi. Panga lililo nolewa
vii. Brush ndogo ya chooni
viii. Fagio ngumu ya chooni (Hard broom)
ix. Rake

N.B Mwanafunzi atatakiwa kuonesha vifaa vilivyoorodheshwa hapo juu siku atakaporipoti shuleni. Nguo na vifaa vyote vya mwanafunzi atakavyotumia binafsi hakikisha vimewekwa alama yakuonekana na isiyofutika kuepusha upotevu.

***ANGALIZO***: Mwanafunzi haruhusiwi kuleta vyakula vya aina yoyote shuleni, nguo za nyumbani, vitu vya thamani kama kamera, radio simu za mkononi, head&earphone, na vitu vinavyoweza kusababisha ajali ya moto kama mishumaa, viberiti, taa za kandili, bangiri, hereni, cheni n.k kama ilivyofafanuliwa kwenye sheria za shule.

**6. AFYA YA WANAFUNZI**

Mwanafunzi mara upatapo barua hii muone mganga wa hospitali ya serikali iliyo karibu na upime afya yako kuthibitisha kuwa una afya ya kumudu masomo, fomu maalum ya kupima afya imeambatishwa. Shule haitoi chakula maalum cha wagonjwa (special diet), hata hivyo mwanafunzi haruhusiwi kuwa na chakula cha aina yoyote bwenini. Mwanafunzi mwenye bima ya afya aje nayo.

***NB: Kuepuka usumbufu wa mwanao kurudishwa nyumbani anapougua, tunashauri kila mwanafunzi akatiwe Bima ya Afya.***

UNAKARIBISHWA SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DAR ES SALAAM.

**...............................**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **MKUU WA SHULE: 0655748374**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE: 0718928181**
- **MAKAMU TAALUMA : 0699460360**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na; **SHERIA ZA SHULE.**

### A. NIDHAMU KWA UJUMLA

1. Wanafunzi wanatakiwa kusimama na kuwasalimia walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yao popote pale wakutanapo na wa aina hiyo.
2. Si ruhusa kupiga kelele, kuzungumza au kusababisha usumbufu wowote ndani na nje ya madarasa.
3. Hairuhusiwi kutumia LUGHA CHAFU miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
4. Wanafunzi wanatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzao, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
5. Wanafunzi wanatakiwa kushirikiana na kutenda kazi yoyote watakayoagizwa kuifanya nje ya madarasa pamoja na kushirikiana katika kazi za elimu ya kujitegemea.
6. Wanafunzi hawaruhusiwi kulewa, kuvuta sigara, kupigana au kuvaa mavazi yenye kuonesha utovu wa nidhamu au kukiuka utamaduni wa mtanzania.
7. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule vikiwemo vitabu, samani au vifaa vya mabwalo, mabweni, madarasa na ofisi. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwa utawala juu ya uharibifu wa mali yoyote ya shule.
8. Wanafunzi wanatakiwa wawe kwenye msitari wakati wa kupewa huduma yoyote.
9. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
10. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au kupewa ruhusa. (i) Nyumba za walimu (ii) Jikoni (iii) Kibanda cha walinzi
11. Ni marufuku kwa wanafunzi kuingia katika sehemu zifuatazo:
    (i) Baa na klabu za usiku
    (ii) Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao.
12. Wawapo shuleni wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama redio, kamera simu za mkononi, seti za runinga na vitu vinavyofanana na hivyo. Mwanafunzi akigundulika kumiliki/kutumia vitu hivyo awapo shuleni atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.
13. Wanafunzi hawaruhusiwi kuleta shuleni vitu vinavyoweza kusababisha ajali ya moto kama mishumaa, viberiti, taa za kandili n.k
14. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na nidhamu nzuri popote pale walipo, ndani na nje ya mazingira ya shule.
15. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu yeyote ambaye sio mwana jumuiya isipokuwa kumsalimia tu.
16. Mwanafunzi akifunga shule au akafukuzwa shule kutokana na tatizo la nidhamu atachukuliwa shuleni na mzazi wake au mlezi aliyethibitishwa na mzazi mwenyewe.

17. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mawasiliano au kupiga simu kwa mzazi bila ruhusa ya utawala, mawasiliano ya muhimu yatanyika kwa kuratibiwa na ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule.

**B. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Aina zote za wizi, unyang'anyi, udanganyifu n.k.
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya.
3. Aina zote za makosa ya kujamiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
4. Kupigana.
5. Makosa ya jinai.
6. Matumizi ya lugha chafu au ya matusi kwa wafanyakazi, wanafunzi wenzake au watu wengineo.
7. Kuolewa au kupata mimba.
8. Uharibifu wa mali ya shule au ya Mwenzake kwa makusudi.
9. Kugoma au kuchochea ghasia.
10. Kuzomea au kumchokoza mwanafunzi au wanafunzi wengine.
11. Kuficha kwa makusudi taarifa ambayo inaweza kusaidia katika kuzuia kutokea kwa jambo baya au la hatari.
12. Kufanya vitendo vinavyohatarisha maisha yake na wengine kama vile kuumiza wenzake kwa makusudi, kutishia kujiua au kuua wengine.
13. Wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mithani na mazoezi ya masomo bila kutoa sababu za kimsingi kwa uongozi wa shule.
14. Kuchelewa kuwasili shuleni kutokea likizoni mara tatu mfululizo bila sababu ya maana.
15. Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa ya utawala.
16. Kulala wawili kitanda kimoja.
17. Kumiliki/kutumia simu na vifaa vinavyoendana na simu ndani ya shule.
18. Kufanya biashara binafsi au ya mtu mwingine shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**MUHIMU:** Fomu zilizoambatanishwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shuleni.

1. Fomu rasmi ya kuandikishwa
2. Ahadi ya mwanafunzi na mzazi/mlezi.
3. Fomu ya uchunguzi wa daktari.
4. Cheti cha kuzaliwa
5. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (IV).

**MAMBO MENGINE YA MUHIMU KUZINGATIA**

## C. KUWAHI.

1. Wanafunzi wanatakiwa kuwahi katika kutekeleza ratiba ya shule.
2. Wanafunzi wanatakiwa kukimbia na kukusanyika jukwaani pindi wakisikia kengele ya yoyote.
3. Wanafunzi wanatakiwa kuwasili kabla ya saa 11:00 jioni. Watakaoshindwa kufanya hivyo bila sababu ya msingi, hawatapokelewa ndani ya uzio wa shule kwa siku hiyo. Wachelewaji kutoka likizoni hawatavumiliwa kwani masomo yetu huanza mara baada ya kufungua shule.
4. Mzazi au mlezi atawajibika kujaza fomu maalum ya kumchukua (wakati anapomchukua) na kumrejesha (wakati anapomrejesha) Mzazi
   /mwanafunzi lazima asaini anaporudi kwa ajili ya kumbukumbu za kiofisi. Mzazi au mlezi asiyefanya hivyo atakuwa amekiuka utaratibu.

## D. UVAAJI WA SARE YA SHULE.

1. Wawapo madarasani
2. Wawapo nje ya shule au wanapohitajika kufanya shughuli rasmi ya kishule.
3. Waendapo hospitali
4. Wawapo safarini kwenda au kutoka likizo.
5. Wanafunzi hawatakiwi kuvaa sare ya shule na viatu virefu na/ au mapambo.
6. Wanafunzi hawatarusiwa kuleta shuleni mapambo.
7. Wanafunzi wanatakiwa kuzingatia usafi kama sehemu muhimu ya maisha yao.
8. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa nadhifu awapo kwenye sare ya shule.
9. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki katika kusafisha mazingira ya shule, madarasa, mabweni na kadhalika pale anapohitajika kufanya hivyo.
10. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie ukaguzi wa usafi ikiwemo sare za shule, usafi wa mwili, vitanda na guo nyingine.
11. Wanafunzi hawaruhusiwi kufuga kucha ndefu.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa nywele mtindo kama kiduku, panki, way n.k.
13. Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele.

## E. MAHUDHURIO

1. Wanafunzi wanatakiwa kuwa madarasani kabla walimu hawajaingia.
2. Ni lazima wanafunzi kuhudhuria shughuli zote ikiwa ni pamoja na vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ya masomo, michezo na mikutano ya shule nzima, madarasani/ mabweni na kazi za nje.

## F. MAANDALIZI YA JIONI NA ASUBUHI

1. Wanafunzi wanatakiwa kuwa madarasani na kujisomea kwa ajili ya maandalizi ya siku inayofuata kuanzia saa moja na nusu (1:30) jioni hadi saa nne (4:30) usiku. Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kupiga kelele au kuwasumbua wenzake wakati wa maandalizi ya asubuhi na jioni.

2. Wanafunzi wanatakiwa kulala ifikapo saa 5:30 usiku. Taa zote za ndani zinatakiwa kuzimwa saa tano na nusu (5:30) usiku isipokuwa za nje, muda huo wanafunzi wote wanatakiwa kuwa vitandani. Wanafunzi wataamka saa kumi na moja kamili asubuhi na kuhudhuria maandalizi ya asubuhi darasani tangu 11:30 hadi saa moja kamili (1:00) asubuhi.

## G. UTENDAJI KITAALUMA

1. Kila mwanafunzi ni lazima ajitume katika masomo tangu anaposajiliwa shuleni hadi anapomaliza shule. Wanafunzi wanakiwa kufanya kazi zote wanazopewa na walimu, mazoezi na mitihani kulingana na kalenda ya shule na ya Baraza la Mitihani la Taifa.
2. Jumamosi ni siku assignment ya wiki, hivyo wanafunzi wote wanatakiwa kuwa darasani tangu saa 2:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana

## H. BWALO

1. Chakula kitagawiwa kila meza kulingana na idadi ya wana meza husika.
2. Bwalo linatakiwa kuwa safi muda wote na kila mwanafunzi atawajibika kuosha vyombo vyake vya chakula.
3. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia, kuchukua chakula jikoni bila ruhusa au kutupa mabaki ya chakula hovyo.
4. Wanafunzi watakula chakula kinachopatikana shuleni tu isipokuwa wataruhusiwa kununua vitafunio vitakavyopatikana hapa shuleni.

## I. MABWENI.

1. Mabweni yote yanatakiwa yawe safi muda wote. Mama mlezi (matron) wa wanafunzi, walimu wa zamu na viranja watafanya ukaguzi wa mabweni. Mashindano ya usafi wa mabweni yatafanyika na bweni litakalopata alama nyingi kwa mwaka mzima litapewa zawadi.
2. Taa zote za chumbani ndani ya mabweni zinatakiwa kuzimwa muda wote wa mchana na baada ya maandalizi ya jioni (5:30 usiku). Hii ni pamoja na kufunga madhubuti mabomba yote ya maji. Feni zote ndani ya chumba zinatakiwa kuwashwa tu wakati wanafunzi wawapo chumbani. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kusomea bwenini wakati wa maandalizi ya jioni.
3. Hairuhusiwi wanafunzi kuwa bwenini wakati wa muda wa kuwa darasani au muda wa maandalizi ya asubuhi au jioni, isipokuwa kwa ruhusa maalum kutoka kwa Matron. Wagonjwa wote watapumzika chumba cha kupumzikia wagonjwa (Sick bay) chini ya uangalizi wa Matron.
4. Ni marufuku kwa wanafunzi kulala wawili katika kitanda kimoja au kulala kwenye bweni/kitanda tofauti na alipopangiwa.
5. Hairuhusiwi mwanafunzi yeyote kuhifadhi dawa. Dawa zote zitahifadhiwa na Matron na wanafunzi wanaolazimika kutumia dawa watapewa dawa hizo na Matron. Wanafunzi hawataruhusiwa kuingiza kemikali za nywele ndani ya shule. Kemikali hizo zikipatikana zitatupwa na mwanafunzi kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

## J. LUGHA YA MAWASILIANO

1. Lugha rasmi ya mawasiliano ndani na nje ya madarasa na kwenye shughuli rasmi ni Kiingereza.

## K. DINI

2. Kila mtu ataruhusiwa kuabudu kwenye dini yake ambayo inafahamika kwa wazazi wake. Kutokana na jiografia ya shule, ibada zote zitafanyika hapa shuleni.
3. Kila mwanafunzi anapaswa kuvumilia tofauti za wengine za kidini. Shule haitavumilia wenye Imani zilizopindukia (religious extremists) ambao wanaweza kuleta madhara kwao wenyewe au kwa wengine kwa kisingizio cha imani.

## L. WAGENI.

1. Wazazi au walezi watawatembelea wanafunzi kwa siku maalum zilizopangwa kama inavyoonyeshwa kwenye kalenda ambayo hupatikana shuleni mwanzoni mwa mwaka wa masomo. Wageni hawaruhusiwi kuingia mabwenini.
2. Wazazi/ walezi hawaruhusiwi kuwatembelea wanafunzi kinyume na utaratibu huo bila sababu za kimsingi. Hata hivyo wanaweza kufanya miadi na walimu wakati wowote kuzungumzia maendeleo ya mwanafunzi kinidhamu na kitaaluma. Iwapo wazazi watakuja shuleni kwa miadi au kwa dharura nyingine yoyote hawataruhusiwa kuingiza shuleni vyakula au vitu vingine vyovyote visivyoruhusiwa ndani ya shule. Iwapo vitu hivyo vitaingizwa shuleni na kukamatwa, shule haitawajibika kuvirudisha na mwanafunzi atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**KIAMBATISHO "A"**

**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA.**

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi: -

PICHA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi……………………………….…………
2. Uraia:…………………………………………..…………………
3. Dini: ……………………………………………………………..
4. Tarehe ya kuzaliwa:…………………………………….…….
5. Mahali ulipozaliwa:…………………………………..……….
6. Yatima/sio yatima/mzazi mmoja (kata isiyohusika)
7. Shule uliyosoma kabla ya kujiunga na shule hii (jaza jedwali).

| JINA ANDIKISHWA SHULENI | SHULE ULIKOTOKA | MWAKA ULIOANZIA | MWAKA ULIOTOKA |
|---|---|---|---|
| | | | |

Saini ya mwanafunzi: ……………………………………………………..

Tarehe………………………………………………….. Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi:

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi:…………………………………………
2. Uraia ……………………………………………………………………
3. Anuani kamili:…………………..……………………………………
4. Sehemu unayoishi Wilaya:……………………..…………………
5. Mtaa:……………………………………………
   Kata:……………………………………………

PICHA YA MZAZI

6. Namba ya simu ..................................... (ya haraka)
7. Jina na mawasiliano ya mlezi wa karibu mjini Dar es Salaam……………………………………
8. Majina manne ya ndugu wa karibu walioidhinishwa kuchukua nafasi ya mzazi/mlezi endapo dharura itatokea:

| Na. | Jina | Uhusiano | Anuani na Anakoishi | Namba ya Simu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

**Maelezo ya kikazi ya Mzazi/Mlezi.**

i. Jina la mwajiri wa Idara……………………………………………………….
ii. Anuani:………………………………………………………………………….
iii. Namba ya simu:……………………………………………………...
iv. Kazi ya Mzazi/Mlezi .............................................. (Mfano: Karani,Mwalimu, Meneja, Mfanyabiashara, Dereva, Mlinzi, Mkulima n.k)

Saini ya Mzazi/Mlezi………………………………………………… Tarehe: ………………………

***NB: Hakikisha unaambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa mwanafunzi.***

**KIAMBATANISHO "B"**

Mimi……………………………………………………………………………………………………

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule hii ya Sekondari

   …………………………………………….Kuanzia tarehe………………………

2. Naahidi kwamba:-

a) Nitazingaitia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu darasani na maktaba ya shule na vifaa vya maabara.

d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi.............................. Tarehe………………….

**KIAMBATANISHO "C"**

**STUDENT"S MEDICAL EXAMINATION FORM**

**TO: THE MEDICAL OFFICER**

HOSPITAL……………………………………………………………………………………………

**Student's**

Name……………………………………………………………………………….Age……………….

Sex ……………………………… Please examine the above named as to

his/her fitness for appointment/re-engagement as a student at

…………………………………………………………………………………………………………………

---

**For UBUNGO MUNICIPAL**
**DIRECTOR MEDICAL**
**CERTIFICATION.**
**(To be completed by Medical Officer)**

**(A) PHYSICAL EXAMINATION**

- Height ………………………………………………………………………..
- Weight……………………………………………………………………..
- Eye sight………………………………………………………………………
- Hearing ……………………………………………………………………..

**(B) PAST HISTORY**

- Heart diseases……………………………………………………………………………
- Drug
- Allergy…………………………………………………………………………
- Asthma……………………………………………………………………………
- Pneumonia……………………………………………………………………………

**(C) LABORATORY TEST**

- Stool……………………………………………………………………………………
- Urine……………………………………………………………………………
- Widal test……………………………………………………………………………
- VRDL……………………………………………………………………………………

- Blood: B/S…………………………………………………………………………………
- Blood Group………………………………………………………………………………...
- Hb………………………………………………………………………………………
- Tuberculosis…………………………………………………………………
- HIV……………………………………………………………………………

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for appointment/re-engagement are as above. Name of Authorized

Doctor………………………………………………………………………

Signature……………………………………………………

Designation…………………………………………………

Date .................................................... Official Stamp

**KIAMBATANISHO "D"**
**VITABUELEKEZI (RECOMMENDED**
**LIST OF BOOKS.**

**01. MATHEMATICS**

i. Pure Mathematics vol 1 ad 2
ii.. Pure Mathematics
iii.Engineering Mathematics iv. Statistics for A- Level v.Understanding Mathematics

**02. PHYSICS**

i. Understanding Physics
ii. Calculation for A-level
iii Chand's principle of Physics

**03. CHEMISTRY.**

i. Chemistry in Action (Freenmentle, M.)
ii. Physical Chemistry
iii. Advanced Chemistry.

**04. BIOLOGY.**

i. Advanced Biology - Principle and Applications
ii. Biological Science - (3rd Edition) by Taylor D Green & stout.
iii. New understanding Biology 4th Edition by Glenn and Susan.
iv. New Biology a functional Approach by Robert M.B

**05. GEOGRAPHY**

i. Geography for Secondary Schools: Form Five. - Tanzania Institute of Education (2016)
ii. Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying. – Zisti Kamili
iii. Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges. – Ahmed Lubwama
iv. A Comprehensive Approach to Physical Geography – D.T. Msabila